



**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**MUHTASARI WA  
TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA, ROBO YA KWANZA  
(JANUARI – MACHI) 2019  
MWAKA WA KIZIO, 2015**



**Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha na Mipango  
Julai, 2019**

Yaliyomo	
Orodha ya Majedwali .....	3
Orodha ya Vielelezo .....	4
Orodha ya Viambatisho .....	4
1.0 Utangulizi .....	6
1.1. Matokeo Muhimu .....	6
1.2. Ukuaji wa Uchumi Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki .....	8
2.0 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi .....	9
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi .....	9
2.1.1 Mazao .....	9
2.1.2 Mifugo .....	10
2.1.3 Misitu .....	10
2.1.4 Uvuvi .....	10
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe .....	10
2.3 Viwanda .....	11
2.4 Umeme .....	11
2.5 Maji Safi na Maji Taka .....	13
2.6 Ujenzi .....	13
2.7 Biashara na Matengenezo .....	14
2.8 Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo .....	14
2.9 Malazi na Huduma ya Chakula .....	14
2.10 Habari na Mawasiliano .....	15
2.11 Fedha na Bima .....	15
2.12 Upangishaji Majengo .....	16
2.13 Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundi .....	16
2.14 Huduma zinazohusiana na Utawala .....	17
2.15 Utawala na Ulinzi .....	17
2.16 Elimu .....	17
2.17 Afya na Huduma za Jamii .....	17
2.18 Sanaa na Burudani .....	18
2.19 Huduma nyingine za kijamii .....	18
2.20 Shughuli za kaya katika kuajiri .....	18
3.0 Hitimisho .....	19

## **Orodha ya Majedwali**

Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini robo ya kwanza kuanzia 2014 – 2019.....	11
--	----

## **Orodha ya Vielelezo**

Kielelezo Namba 1: Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza, kuanzia 2014 - 2019.....	7
Kielelezo 2: Mchango wa shughuli za uchumi kwa Bei za Miaka husika.....	7
Kielelezo 3: Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Januari - Machi, 2014 - 2019, – 2019.....	8
Kielelezo Na 4: Ukuaji wa Uchumi wa Nchi Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.....	9
Kielelezo Na 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza ya Mwaka 2018 na 2019.....	10
Kielelezo Na. 6: Mgawanyo Umeme Kutokana na Aina ya Chanzo, Januari - Machi 2019.....	13
Kielelezo 7: Uumeme Uliozalishwa (Milioni kWh) na Ukuaji, Robo ya Kwanza 2014 - 2019.....	14
Kielelezo 8: Maji yaliyozalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Januari– Machi 2014 – 2019.....	15
Kielelezo Na. 9: Mauzo ya Huduma za Mawasiliano Kutoka kwa Watoa Huduma, Robo ya Kwanza Mwaka 2014 – 2019.....	17
kielelezo 10: Kiasi cha Mikopo na Amana za Wateja (Sh. Trilioni) Januari - Machi 2015 - 2019....	18

## **Orodha ya Viambatisho**

Kiambatisho Na .1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni 20

Kiambatisho Na..2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi Bei za mwaka 2015 – katika asilimia .....	22
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni .....	24
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi kwa Pato la Taifa Kwa Bei Za Soko (Bei za miaka inayohusika) -katika asilimia.....	26

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari huu unatoa taarifa ya Pato la Taifa kwa bei za miaka husika na mwaka wa kizio wa 2015 kwa Tanzania Bara. Taarifa ya Pato la Taifa ya kila robo mwaka hutumika kutathimini mabadiliko ya kiuchumi katika vipindi vifupi hivyo kuwezesha kufanya afua za sera za uchumi kwa wakati.


Taarifa zilizotumika kutayarisha takwimu za Pato la Taifa, robo ya kwanza (Januari-Machi) ya Mwaka 2019 zilikusanywa kutoka katika shughuli zote za uchumi za uzalishaji wa bidhaa na huduma zilizofanyika nchini. Aidha, ukokotoaji umezingatia miongozo ya Umoja wa Mataifa ya Ukokotoaji wa Takwimu ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Pato la Taifa ujulikanao kama *System of National Accounts 2008*.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilianza kutekeleza Sera ya Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa mwanzoni mwa mwaka 2019. Sera hii inatoa fursa ya kuchapisha matokeo ya awali ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisho kulingana na upatikanaji wa takwimu mpya za kila robo mwaka na za kila mwaka.

### 1.1. Matokeo Muhimu


Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa na thamani ya shilingi milioni 33,709,171 ikilinganishwa na shilingi milioni 32,132,681 za robo ya kwanza ya mwaka 2018. Aidha, thamani ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 iliongezeka hadi shilingi milioni 30,019,412 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 kutoka shilingi milioni 28,173,964 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, sawa na ukuaji wa asilimia 6.6.

**Kielelezo Namba 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Kuanzia 2014 - 2019**




Mchango wa shughuli kuu za kiuchumi za Msingi (*primary activities*) ambazo zinajumuisha kilimo, mifugo, misitu, uvuvi na uchimbaji madini ulikuwa asilimia 36 katika Pato la Taifa. Mchango wa shughuli kuu za Kiuchumi za Kati (*secondary activities*) ambazo zinajumuisha Uzalishaji viwandani, Ujenzi, Umeme na Maji ulikuwa asilimia 24, wakati mchango wa shughuli kuu za Utoaji wa Huduma (*tertiary activities*) ambazo ni pamoja na biashara, usafirishaji na huduma za fedha na bima ulikuwa asilimia 40. Mchango wa shughuli kuu za kiuchumi umekokotolewa kabla ya kujumuisha thamani ya kodi katika bidhaa na huduma.

**Kielelezo 2: Mchango wa Shughuli Kuu za Uchumi kwa Bei za Miaka husika**



Katika kipindi hicho, shughuli ya Ujenzi iliongoza kwa kasi kubwa ya ukuaji ya asilimia 13.2 ikifuatiwa na shughuli ya usafirishaji na Uhifadhi Mizigo asilimia 11.1 na shughuli ya Uchimbaji wa Madini na Mawe asilimia 10.0.


**Kielelezo 3: Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo Mwaka ya Kwanza (Januari-Machi) 2019,**



### 1.2. Ukuaji wa Uchumi Kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ulionyesha kuwa: uchumi wa Rwanda uliongezeka kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 10.4 mwaka 2018 hii ikiwa ni kupungua kwa kasi kwa pointi 2.0 za asilimia. Uchumi wa Uganda uliongezeka kwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2018 ikiwa ni kupungua kwa kasi kwa pointi 1.3 ya asilimia. Uchumi wa Kenya ulikua kwa asilimia 5.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.5 katika robo ya kwanza ya 2018 ikiwa ni kupungua kwa kasi kwa pointi 0.9 ya asilimia. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, Nchi zote katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekuwa na kasi ndogo ya ukuaji ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2018. Makadirio ya Pato la Taifa kwa Nchi za Burundi na Sudani Kusini bado hayajatolewa.

**Kielelezo Na 4: Ukuaji wa Uchumi Katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**





## 2.0 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi

### 2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hii inahusisha uvunaji wa rasilimali za asili za mboga mboga za majani na wanyama zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka mashamba ya ufugaji au mazingira yao ya asili.

#### 2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, Mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharage na mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, korosho, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na mazao ya biashara.

Shughuli ya uzalishaji wa mazao iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 8.9 ya robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na upatikanaji wa mvua za kutosha katika maeneo ya uzalishaji wakati wa msimu wa vuli.

**Kielelezo Na 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Kwanza ya Mwaka 2019 na 2018**



Mazao ambayo yalichangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa shughuli ya mazao ni pamoja na mahindi ambayo yaliongezeka kwa asilimia 2.1 kutoka tani milioni 2.629 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi tani milioni 2.686 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019. Viazi vitamu viliongezeka kwa asilimia 24.2 kutoka tani elfu 231

katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi tani elfu 287 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019. Maharage na jamii ya mikunde yaliongezeka kwa asilimia 3.7 kutoka tani elfu 142 mwaka 2018 hadi tani elfu 147 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019. Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 48.5 kutoka tani elfu 31 robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi tani elfu 46 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ulezi/Mtama uliongezeka kwa asilimia 1.0 kutoka tani elfu 396 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi tani elfu 400 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019.

### **2.1.2 Mifugo**

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi; kondoo; punda na farasi; nguruwe, sungura; kuku wa kienyeji na kisasa; na kuku wa aina nyingine.

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2019, Shughuli za mifugo ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.9 sawa na kasi ya robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za mifugo ambazo ziliongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeko kwa pato la wastani la mwananchi, kupanuka kwa miji, pamoja na kuongezeka kwa ufahamu juu ya lishe bora.

### **2.1.3 Misitu**

Shughuli hii inahusisha uzalishaji wa mbao, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyigine zisizo za miti. Shughuli za misitu ziliongezeka kiwango cha asilimia 4.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa juhudi za Serikali katika usimamizi wa rasilimali za misitu na kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

### **2.1.4 Uvuvi**

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi kutoka baharini, maziwa na mito. Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 17.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia hasi 2.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uvunaji wa mazao ya samaki.

## **2.2 Uchimbaji Madini na Mawe**

Uchimbaji madini na mawe unahusisha uchimbaji wa madini kama vile makaa ya mawe, vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Uchimbaji wa madini hufanyika chini ya ardhi, juu ya ardhi au kwenye visima. Pia unajumuisha shughuli za ziada zenye lengo la kuandaa madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha, kukausha, kuchambua, n.k. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilipo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji madini na mawe imegawanywa katika makundi manne ambayo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2019, shughuli ya Uchimbaji wa Madini na Mawe iliongezeka kwa kasi ya asilimia 10.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia hasi 5.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu, makaa ya mawe, na almasi.

**Jedwali Na 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Kwanza Kuanzia Mwaka 2014 – 2019**

Madini	Kipimo	2014	2015	2016	2017	2018	2019
Makaa ya Mawe	Tani	49,377	61,085	38,704	128,712	129,873	205,045
Almasi	Karati	94,278	72,086	77,959	69,897	97,497	117,187
Dhahabu	Kilo	10,711	10,458	10,596	10,699	8,655	8,656
Chumvi	Tani	16,584	25,807	37,248	40,486	22,141	31,321
Fedha	Kilo	2,524	3,435	4,162	3,488	1,973	2,856
Gesi Asilia	Mscf	8,757	8,117	11,980	12,710	13,729	16,138

### 2.3 Viwanda

Shughuli ya Uzalishaji Viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa katika hali yake ya awali na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumiwa na mlaji kama bidhaa za mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwanda.


Shughuli ya Uzalishaji Viwandani iliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwanda kwa jumla.

### 2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Shughuli hii ni mahsusi katika uzalishaji wa umeme kutokana na vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Pia inashughulika na usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za shughuli hii ni makampuni ya uzalishaji wa umeme.


Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2019, umeme uliozalishwa uliongezeka hadi kWh milioni 1,944 kutoka kWh milioni 1,752 zilizozalishwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Umeme uliozalishwa kutokana na nishati ya gesi ulikuwa asilimia 79 ya umeme wote uliozalishwa katika robo ya kwanza ya mwaka 2019. Vyanzo vingine vilikuwa umeme wa maji asilimia 20 na asilimia 1 iliyobaki ilitokana na umeme wa mafuta.

**Kielelezo 6: Mgawanyo wa Umeme Uliozalishwa kwa Aina ya Chanzo, Januari- Machi, 2019**



Ukuaji wa shughuli ya umeme hutegemea kiasi cha umeme uliozalishwa na kusambazwa kwa watumiaji. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, umeme uliozalishwa uliongezeka hadi kWh milioni 1,944 kutoka kWh milioni 1,752 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Katika kipindi hicho, kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 9.7 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 0.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018.

**Kielelezo 7: Umeme Uliozalishwa na Kasi ya ukuaji, Robo ya Kwanza, Mwaka of 2014 - 2019**




## 2.5 Maji Safi na Maji Taka

Shughuli hii inahusika na ukusanyaji na usafishaji wa maji kwa ajili ya usambazaji, Aidha, inahusika na kusafisha maji ya bahari ili kuondoa chumvi kwa ajili ya kuzalisha maji ya kutumia na kukusanya maji moja kwa moja kutoka visima kwa matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya.

Ukuaji wa shughuli ya maji inategemea wingi wa maji yaliyozozalishwa. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2019, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 64.6 kutoka mita za ujazo milioni 59.3 zilizozalishwa katika robo ya kwanza mwaka 2018.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 8.0 ikilinganishwa na asilimia 3.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya uzalishaji wa maji na kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha maji ili kukidhi mahitaji ya maji kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu hususan katika maeneo ya mijini ili kuendena na ongezeko la mahitaji ya maji.

**Kielelezo 8: Maji yaliyozalishwa (Mita za Ujazo Milioni), Januari hadi Machi, 2014 – 2019**



## 2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa jumla na shughuli maalumu za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii pia inajumuisha kazi mpya za ujenzi, ukarabati, marekebisho makubwa kwenye majengo, na ujenzi wa miundo mbinu.

Ujenzi wa jumla ni ujenzi wa nyumba nzima, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma, miundombinu ya mashamba n.k., pia inajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, na mifumo ya umeme, viwanja vya michezo n.k.

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 13.2, ikilinganishwa na asilimia 15.6 katika robo ya kwanza ya mwaka ya 2018. Ukuaji ulitokana na ongezeko la uzalishaji wa vifaa vya ujenzi vilivyozalishwa ndani ya Nchi kama vile saruji na vyuma ambavyo vinatumika katika shughuli za ujenzi.

## **2.7 Biashara na Matengenezo**

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na uuzaji wa rejareja (uuzaji wa bidhaa bila kuongeza thamani) ya aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji na ukarabati wa bidhaa za kibinafsi na za nyumbani. Shughuli hii inahusisha kununua na kuuza bidhaa. Shughuli ya Uuzaji wa jumla na rejareja ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la bidhaa za biashara hasa bidhaa za kilimo na bidhaa za viwandani.

## **2.8 Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo**

Shughuli hii inahusika na huduma ya usafiri wa abiria au mizigo, unaozingatia ratiba maalum za safari au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana kama vile utunzaji, uhifadhi wa mizigo n.k. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri pamoja na dereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Shughuli ya Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 11.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 8.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la idadi ya abiria na mizigo waliosafirishwa katika kipindi hicho.

## **2.9 Malazi na Huduma ya Chakula**

Shughuli hii inajumuisha huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.


Huduma za malazi na chakula ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji huu mdogo ulitokana na kupungua kwa idadi ya watalii na ongezeko dogo la vitanda vilivyotumika kulala wageni katika kipindi hicho. Idadi ya watalii walikuwa 334,460 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na 356,731 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018.

## 2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji wa vitabu, upigaji picha za kawaida, video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji, kwa mfano, utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari za uchakataji wa data.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 9.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 14.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la muda wa maongezi uliotumiwa na wateja wa simu za mkononi na kuongezeka kwa huduma za utangazaji na mtandao.


**Kielelezo Na. 9: Mauzo ya Huduma za Mawasiliano Katika Robo ya Kwanza, Mwaka 2014 – 2019**



## 2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusu utoaji wa huduma za kifedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za kifedha. Shughuli ya fedha na bima ilikua kwa kasi ya asilimia 5.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia hasi 2.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na ongezeko la asilimia 4.9 katika amana kutoka shilingi trilioni 19.57 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi shilingi trilioni 20.52 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 na pia ongezeko la asilimia 11.1 katika kiwango cha mikopo kutoka shilingi trilioni 16.14 robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi shilingi trilioni 17.94 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019; na pia kuongezeka kwa huduma za bima.

**Kielelezo Na. 1: Kiasi cha Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Januari hadi Machi, 2015 - 2019**



### **2.12 Upangishaji Majengo**

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha majengo, kutoa huduma nyingine ya mali isiyohamishika.

Kiwango cha ukuaji kilikuwa asilimia 4.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 4.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la mahitaji ya malazi hususan katika maeneo ya mijini.

### **2.13 Shughuli za Kitalaam, Sayansi na Ufundi**

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalumu za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalumu utakaotumika kutoa huduma kwa watumiaji.

Shughuli hii inajumuisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; upimaji na uchambuzi wa kiutaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa soko; utaalamu wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 6.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 12.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la mahitaji ya shughuli za kitaaluma, kisheria na uhasibu.



## **2.14 Huduma zinazohusiana na Utawala**

Shughuli hii inahusika na huduma mbalimbali zinazosaidia shughuli za biashara kufanyika. Huduma za utawala zinahusisha huduma za kukodisha vifaa; ajira; huduma za mashirika ya usafiri, huduma za kuongoza watalii, huduma za kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana; usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji kiliongezeka kwa asilimia 8.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la huduma za wakala wa kusafirisha abiria na shughuli za makapuni ya kuongoza watalii.

## **2.15 Utawala na Ulinzi**

Shughuli hii inahusika na kutunga na kutafisiri sheria, kodi, ulinzi, usalama wa raia, huduma za uhamiaji, na uendeshaji wa serikali. Shughuli hii inajumuisha pia huduma za mifuko ya lazima ya hifadhi ya jamii.

Katika robo ya kwanza ya mwaka 2019, kiwango cha ukuaji kiliongezeka kwa asilimia 2.7 ikilinganishwa na asilimia 8.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na ongezeko la matumizi ya serikali katika sekta za huduma na utawala na ulinzi.

## **2.16 Elimu**

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Aidha, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali zilizopo katika mfumo rasmi wa shule katika ngazi tofauti tofauti pamoja na elimu ya watu wazima, elimu ya kujifunza kusoma na kuandika n.k. Shughuli hii inajumuisha taasisi za elimu za umma na binafsi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 11.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi na sekondari pamoja na ongezeko la matumizi ya Serikali katika Sekta ya elimu.

## **2.17 Afya na Huduma za Jamii**

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na huduma za jamii. Huduma hizo ni pamoja na zinazotolewa na wataalam wa matibabu walioelimishwa katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha

shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalamu wa huduma za afya.

Shughuli za afya ziliongezeka kwa kiwango cha asilimia hasi 2.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa asilimia 17.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kupungua kwa idadi ya wagonjwa walihudumiwa katika vituo vya afya vya binafsi kutoka 2,617,837 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018 hadi kufikia 2,390,253 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019.

### **2.18 Sanaa na Burudani**

Shughuli hii inajumuisha shughuli mbalimbali zinazotolewa ili kutoa burudani kwa umma na kukidhi maslahi mbalimbali ya kitamaduni. Huduma nyingine ni utoaji wa burudani za bendi, uendeshaji wa maeneo ya makumbusho, kamari, huduma za michezo na burudani kwa ujumla.

Kiwango cha ukuaji kilikua kwa asilimia 7.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 12.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Ukuaji ulitokana na ongezeko la shughuli za kisanii na burudani.

### **2.19 Huduma nyingine za kijamii**

Shughuli hii inahusisha uanachama katika taasisi na mashirika ya kijamii, ukarabati wa kompyuta na bidhaa za kibinafsi na za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za kibinafsi ambazo hazijajumuishwa kwenye makundi mengine kama zilivyoainishwa katika shughuli za kiuchumi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.6 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 ikilinganishwa na asilimia 8.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la idadi ya watu mijini na shughuli za kibinafsi.

### **2.20 Shughuli za kaya katika kuajiri**

Shughuli za kaya katika kuajiri zinajumuisha wafanyakazi wa ndani kama vile wapishi, wahudumu, wafugaji, wataalamu wa bustani, wakulima, walinzi wa mlangoni, waendeshaji wa gari, waangalizi wa watoto, wafundishaji, wafugaji, makarani n.k. Bidhaa zinazozalishwa katika shughuli hii hutumiwa na kaya inayoajiri.

Shughuli hii ilikua kwa kiwango cha asilimia 3.1 katika robo ya kwanza ya mwaka 2019 sawa na kiwango cha ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji kilitokana na ongezeko la wakazi mijini.

### **3.0 Hitimisho**

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2019, Pato la Taifa liliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.6 ikilinganishwa na asilimia 7.5 mwaka 2018. Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya tarakimu mbili katika kipindi hicho zilikuwa Ujenzi (asilimia 13.2); Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 11.1), na Uchimbaji wa Madini na Mawe (asilimia 10.0).

Kwa mujibu wa Sera ya Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwanzoni mwa mwaka 2019, takwimu za Pato la Taifa, robo ya kwanza mwaka 2019, zinaweza kurekebishwa kutokana na upatikanaji wa taarifa mpya ambazo hazikupatikana wakati wa kukokotoa Pato la Taifa, au masahihisho ya taarifa zilizotumika yaliyofanyika kutoka kwenye vyanzo vya taarifa hizo.

**Kiambatisho Na.1: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

Mwaka	Robo mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengen ezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Usafirisha ji na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		21,807,030	3,314,742	6,066,989	669,069	358,361	7,578,263	7,371,411	1,343,924	5,710,466	1,266,747	3,444,161
2013		22,408,192	3,464,721	6,292,514	723,608	367,890	9,023,353	7,682,286	1,356,204	6,050,976	1,414,116	3,405,940
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		28,008,976	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,821,248	1,525,619	7,815,845	1,824,471	4,115,393
2018		29,482,834	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,546,664	10,395,783	1,604,391	8,736,561	1,989,829	4,094,972
2012	1	5,972,854	845,470	1,528,195	151,473	86,422	1,816,993	1,877,418	321,003	1,208,445	281,981	849,590
2012	2	5,182,996	825,383	1,544,666	164,427	89,319	1,808,760	1,855,404	320,427	1,456,176	303,507	844,631
2012	3	4,092,001	833,592	1,499,895	172,946	92,526	2,012,312	1,725,714	358,248	1,489,645	327,526	886,247
2012	4	6,559,178	810,297	1,494,233	180,223	90,094	1,940,197	1,912,875	344,245	1,556,199	353,733	863,692
2013	1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
2013	2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
2013	3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
2013	4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
2014	1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
2014	2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
2014	3	4,450,294	929,381	1,788,128	213,998	97,099	2,228,708	2,035,245	361,470	1,686,150	414,058	960,721
2014	4	7,289,215	948,546	1,803,489	216,605	102,059	2,334,808	2,280,578	350,362	1,649,417	422,793	963,401
2015	1	6,605,887	923,326	1,733,636	211,828	96,862	2,438,046	2,093,973	346,778	1,654,599	386,446	995,846
2015	2	6,347,239	965,335	1,820,111	199,281	92,862	2,690,105	2,195,254	345,054	1,676,064	412,841	1,011,653
2015	3	4,656,388	960,427	1,939,664	192,215	99,585	2,601,253	2,162,776	372,080	1,764,202	441,478	1,076,143
2015	4	7,625,045	1,206,532	1,918,260	195,477	101,448	2,717,393	2,295,860	358,003	1,835,030	440,334	1,105,380
2016	1	6,788,342	1,017,609	1,965,656	214,850	95,779	2,859,933	2,295,506	358,142	1,818,390	401,047	1,111,056
2016	2	6,853,095	1,109,064	1,996,019	210,034	100,816	2,995,869	2,318,553	347,167	1,819,827	421,552	1,052,954
2016	3	4,936,684	1,098,979	2,080,908	214,673	103,584	3,208,669	2,300,383	385,323	1,854,653	451,160	1,053,955
2016	4	7,858,218	1,131,055	2,170,783	229,706	117,720	2,896,249	2,346,262	389,420	1,831,986	444,789	1,017,550
2017	1	7,233,097	1,118,373	2,067,899	223,751	97,295	3,204,078	2,338,470	374,854	1,914,669	452,123	1,046,585
2017	2	7,283,729	1,057,691	2,187,504	207,413	105,045	3,631,267	2,437,212	359,355	1,910,951	449,234	1,028,221
2017	3	5,139,926	1,144,597	2,365,766	222,988	113,969	3,198,026	2,434,360	395,146	1,982,315	459,555	997,959
2017	4	8,352,224	1,267,964	2,268,650	223,515	128,352	3,731,635	2,611,207	396,263	2,007,909	463,560	1,042,628
2018	1	7,701,080	1,054,655	2,176,664	225,628	100,913	3,703,467	2,437,985	391,664	2,082,426	519,325	1,016,363
2018	2	7,727,079	1,129,287	2,266,799	221,519	111,470	3,821,155	2,533,895	383,333	2,169,733	504,727	1,004,878
2018	3	5,336,655	1,166,716	2,532,462	235,515	126,137	3,644,053	2,602,690	425,407	2,222,813	481,637	1,036,662
2018	4	8,718,021	1,308,537	2,647,575	245,512	138,991	4,377,990	2,821,212	403,987	2,261,589	484,140	1,037,069
2019	1	8,182,587	1,159,804	2,280,570	247,584	108,984	4,193,881	2,531,422	396,098	2,312,794	568,958	1,073,226
2019												
2019												
2019												

**Kiambatisho Na. 1 (kinaendelea): Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni**

Mwaka	Robo mwaka	Utawala na Ulinzi	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	Huduma zinazohusiana na Utawala	Upangishaji Majengo	Elimu	Afya na Huduma za Jami	Huduma nyingine za Kijamii	Jumla ya Ongezeko la Thamani	Ogeza kodi katika bidhaa	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko
2012		3,623,123	322,260	1,417,467	2,606,439	1,922,643	1,284,594	910,388	71,018,076	6,961,771	77,979,847
2013		3,974,206	385,090	1,660,994	2,714,775	1,927,633	1,245,030	991,460	75,088,988	8,179,129	83,268,117
2014		4,242,164	447,921	1,976,260	2,828,970	2,186,260	1,349,941	1,088,317	80,873,021	8,001,090	88,874,111
2015		4,548,604	518,123	2,183,917	2,949,598	2,413,306	1,419,090	1,144,099	86,484,736	7,864,579	94,349,316
2016		4,793,820	606,207	2,611,498	3,077,086	2,665,336	1,497,896	1,278,046	92,803,857	8,024,535	100,828,393
2017		4,907,113	694,291	2,892,463	3,211,895	2,859,171	1,611,999	1,409,504	99,263,761	8,393,644	107,657,405
2018		5,058,292	763,332	3,054,288	3,354,518	3,046,789	1,742,444	1,516,831	106,075,908	9,064,286	115,140,194
2012	1	803,642	74,831	340,487	641,698	461,652	309,228	217,530	17,788,914	1,732,167	19,521,081
	2	817,057	78,603	347,905	648,276	447,191	320,506	221,443	17,276,676	1,596,603	18,873,279
	3	976,077	82,451	358,076	654,899	505,099	339,618	234,892	16,641,764	1,737,034	18,378,797
	4	1,026,348	86,375	371,000	661,566	508,702	315,242	236,523	19,310,723	1,895,967	21,206,689
2013	1	897,436	90,376	386,679	668,325	454,979	299,454	239,370	18,443,971	1,947,582	20,391,553
	2	945,222	94,335	404,378	675,175	462,904	314,552	240,745	18,180,405	1,975,657	20,156,062
	3	1,061,729	98,252	424,098	682,119	501,425	323,848	253,497	17,755,599	2,088,269	19,843,868
	4	1,069,818	102,128	445,840	689,157	508,325	307,176	257,849	20,709,012	2,167,622	22,876,634
2014	1	1,007,519	105,963	469,602	696,292	510,028	322,658	266,230	20,026,099	2,102,819	22,128,918
	2	1,022,325	109,904	488,892	703,526	525,815	342,267	268,409	20,039,997	1,866,580	21,906,577
	3	1,105,719	113,951	503,710	710,859	571,648	346,149	276,932	18,794,219	1,989,729	20,783,948
	4	1,106,601	118,104	514,055	718,293	578,769	338,867	276,745	22,012,706	2,041,962	24,054,668
2015	1	1,033,818	122,364	519,928	725,830	557,686	331,321	277,986	21,056,161	1,721,421	22,777,583
	2	1,067,508	126,934	532,698	733,472	573,927	344,848	279,553	21,414,740	1,952,108	23,366,848
	3	1,227,874	131,816	552,364	741,220	640,405	377,131	291,033	20,228,053	2,137,973	22,366,026
	4	1,219,405	137,009	578,927	749,076	641,287	365,789	295,528	23,785,782	2,053,077	25,838,859
2016	1	1,236,354	142,513	612,386	757,042	672,749	383,295	303,604	23,034,254	1,945,089	24,979,343
	2	1,233,036	148,330	641,965	765,119	676,794	383,518	309,726	23,383,437	1,904,859	25,288,296
	3	1,152,150	154,460	667,664	773,310	651,053	361,396	326,868	21,775,874	2,059,788	23,835,662
	4	1,172,280	160,904	689,482	781,616	664,740	369,687	337,848	24,610,293	2,114,799	26,725,092
2017	1	1,170,477	165,581	702,756	790,039	682,943	384,182	340,656	24,307,828	1,895,232	26,203,060
	2	1,240,969	170,998	716,993	798,581	716,119	410,270	344,216	25,055,766	1,917,164	26,972,929
	3	1,238,523	176,281	730,234	807,244	724,346	401,418	359,004	22,891,656	2,145,194	25,036,850
	4	1,257,145	181,430	742,480	816,031	735,762	416,129	365,629	27,008,511	2,436,054	29,444,565
2018	1	1,273,252	186,445	739,367	824,942	759,760	451,212	370,331	26,015,480	2,158,485	28,173,964
	2	1,232,622	190,206	755,504	833,980	745,747	434,439	373,257	26,439,629	2,185,863	28,625,492
	3	1,272,839	192,714	771,641	843,148	768,623	431,449	387,040	24,478,200	2,339,793	26,817,993
	4	1,279,580	193,967	787,778	852,447	772,659	425,344	386,202	29,142,600	2,380,145	31,522,745
2019	1	1,307,326	198,739	803,746	861,880	787,359	441,674	391,363	27,847,996	2,171,416	30,019,412

**Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi Bei za mwaka 2015 – katika Asilimia**

Mwaka	Robo mwaka	Kilimo	Uchimbaji i Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na Maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya chakula	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	Habari na Mawasilian	Fedha na Bima
2013		2.8	4.5	3.7	8.2	2.7	19.1	4.2	0.9	6.0	11.6	-1.1
2014		6.9	6.4	10.0	12.7	3.8	2.5	9.9	3.1	8.7	10.3	10.5
2015		5.4	10.0	7.1	-2.0	2.4	12.9	3.6	1.7	5.4	7.8	11.3
2016		4.8	7.4	10.8	8.8	6.9	14.5	5.9	4.1	5.7	2.2	1.1
2017		5.9	5.3	8.2	1.0	6.4	15.1	6.1	3.1	6.7	6.2	-2.8
2018		5.3	1.5	8.3	5.8	7.4	12.9	5.8	5.2	11.8	9.1	-0.5
2012	1	1.8	13.5	5.9	-4.1	2.6	4.2	9.1	3.1	-0.4	29.7	4.5
	2	-0.3	11.3	0.6	0.1	2.8	-0.3	1.3	3.9	17.0	26.2	4.3
	3	0.8	-0.1	-0.5	12.8	5.7	7.5	-3.2	8.9	3.2	21.5	6.2
	4	0.3	8.4	-6.1	6.6	0.3	1.1	-6.6	6.1	12.2	16.1	8.8
2013	1	0.4	-11.5	-4.5	10.6	1.0	18.2	-2.6	3.6	25.7	10.7	-4.5
	2	3.7	3.0	0.2	7.6	0.8	16.8	1.6	1.3	3.1	13.0	-1.0
	3	2.6	5.0	11.9	4.9	-7.1	18.8	9.7	-1.2	1.6	9.4	-0.5
	4	4.2	22.2	7.6	9.7	16.1	22.4	8.6	0.2	-2.5	13.2	1.5
2014	1	5.7	25.3	11.1	20.5	0.7	1.7	12.4	4.3	7.0	9.8	12.4
	2	9.3	2.5	10.3	3.3	5.2	18.7	10.1	4.5	7.7	10.9	10.9
	3	6.0	6.2	6.6	17.9	13.0	-6.7	7.5	2.1	11.4	15.5	9.0
	4	6.6	-4.2	12.1	9.6	-2.4	-1.7	9.8	1.6	8.7	5.6	9.9
2015	1	4.3	-1.5	6.9	4.9	10.2	11.7	1.9	0.0	1.8	12.7	9.2
	2	8.0	10.7	6.6	9.0	-1.9	7.3	5.8	1.7	3.7	8.6	9.0
	3	4.6	3.3	8.5	-10.2	2.6	16.7	6.3	2.9	4.6	6.6	12.0
	4	4.6	27.2	6.4	-9.8	-0.6	16.4	0.7	2.2	11.3	4.1	14.7
2016	1	2.8	10.2	13.4	1.4	-1.1	17.3	9.6	3.3	9.9	3.8	11.6
	2	8.0	14.9	9.7	5.4	8.6	11.4	5.6	0.6	8.6	2.1	4.1
	3	6.0	14.4	7.3	11.7	4.0	23.4	6.4	3.6	5.1	2.2	-2.1
	4	3.1	-6.3	13.2	17.5	16.0	6.6	2.2	8.8	-0.2	1.0	-7.9
2017	1	6.6	9.9	5.2	4.1	1.6	12.0	1.9	4.7	5.3	12.7	-5.8
	2	14.8	-4.6	9.6	-1.2	4.2	21.2	5.1	3.5	5.0	6.6	-2.3
	3	4.1	4.2	13.7	3.9	10.0	-0.3	5.8	2.5	6.9	1.9	-5.3
	4	6.3	12.1	4.5	-2.7	9.0	28.8	11.3	1.8	9.6	4.2	2.5
2018	1	6.5	-5.7	5.3	0.8	3.7	15.6	4.3	4.5	8.8	14.9	-2.9
	2	6.1	6.8	3.6	6.8	6.1	5.2	4.0	6.7	13.5	12.4	-2.3
	3	3.8	1.9	7.0	5.6	10.7	13.9	6.9	7.7	12.1	4.8	3.9
	4	4.4	3.2	16.7	9.8	8.3	17.3	8.0	1.9	12.6	4.4	-0.5
2019	1	6.3	10.0	4.8	9.7	8.0	13.2	3.8	1.1	11.1	9.6	5.6

**Kiambatisho Na. 2 (kinaendelea) Ukuaji wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi Bei za mwaka 2015 – katika asilimia**

Mwaka	Robo mwaka	Utawala na Ulinzi	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	Huduma zinazohusiana na Utawala	Upangishaji Majengo	Elimu	Afya na Huduma za Jamii	Huduma nyingine za Kijamii	Jumla ya Ongezeko la Thamani	Ongeza kodi katika bidhaa	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko
2013		9.7	19.5	17.2	4.2	0.3	-3.1	8.9	5.7	17.5	6.8
2014		6.7	16.3	19.0	4.2	13.4	8.4	9.8	7.7	-2.2	6.7
2015		7.2	15.7	10.5	4.3	10.4	5.1	5.1	6.9	-1.7	6.2
2016		5.4	17.0	19.6	4.3	10.4	5.6	11.7	7.3	2.0	6.9
2017		2.4	14.5	10.8	4.4	7.3	7.6	10.3	7.0	4.6	6.8
2018		3.1	9.9	5.6	4.4	6.6	8.1	7.6	6.9	8.0	7.0
2012	1	-11.6	28.4	11.3	4.1	-0.1	-6.0	11.0	3.4	-0.1	3.1
	2	-5.4	25.0	9.2	4.1	-2.1	-5.9	10.4	2.6	-11.1	1.3
	3	22.3	22.8	9.0	4.1	11.7	7.6	12.0	4.2	-6.3	3.1
	4	28.4	21.4	10.5	4.1	12.2	10.6	11.1	3.2	3.4	3.2
2013	1	11.7	20.8	13.6	4.1	-1.4	-3.2	10.0	3.7	12.4	4.5
	2	15.7	20.0	16.2	4.1	3.5	-1.9	8.7	5.2	23.7	6.8
	3	8.8	19.2	18.4	4.2	-0.7	-4.6	7.9	6.7	20.2	8.0
	4	4.2	18.2	20.2	4.2	-0.1	-2.6	9.0	7.2	14.3	7.9
2014	1	12.3	17.2	21.4	4.2	12.1	7.7	11.2	8.6	8.0	8.5
	2	8.2	16.5	20.9	4.2	13.6	8.8	11.5	10.2	-5.5	8.7
	3	4.1	16.0	18.8	4.2	14.0	6.9	9.2	5.8	-4.7	4.7
	4	3.4	15.6	15.3	4.2	13.9	10.3	7.3	6.3	-5.8	5.1
2015	1	2.6	15.5	10.7	4.2	9.3	2.7	4.4	5.1	-18.1	2.9
	2	4.4	15.5	9.0	4.3	9.2	0.8	4.2	6.9	4.6	6.7
	3	11.0	15.7	9.7	4.3	12.0	9.0	5.1	7.6	7.5	7.6
	4	10.2	16.0	12.6	4.3	10.8	7.9	6.8	8.1	0.5	7.4
2016	1	19.6	16.5	17.8	4.3	20.6	15.7	9.2	9.4	13.0	9.7
	2	15.5	16.9	20.5	4.3	17.9	11.2	10.8	9.2	-2.4	8.2
	3	-6.2	17.2	20.9	4.3	1.7	-4.2	12.3	7.7	-3.7	6.6
	4	-3.9	17.4	19.1	4.3	3.7	1.1	14.3	3.5	3.0	3.4
2017	1	-5.3	16.2	14.8	4.4	1.5	0.2	12.2	5.5	-2.6	4.9
	2	0.6	15.3	11.7	4.4	5.8	7.0	11.1	7.2	0.6	6.7
	3	7.5	14.1	9.4	4.4	11.3	11.1	9.8	5.1	4.1	5.0
	4	7.2	12.8	7.7	4.4	10.7	12.6	8.2	9.7	15.2	10.2
2018	1	8.8	12.6	5.2	4.4	11.2	17.4	8.7	7.0	13.9	7.5
	2	-0.7	11.2	5.4	4.4	4.1	5.9	8.4	5.5	14.0	6.1
	3	2.8	9.3	5.7	4.4	6.1	7.5	7.8	6.9	9.1	7.1
	4	1.8	6.9	6.1	4.5	5.0	2.2	5.6	7.9	-2.3	7.1
2019	1	2.7	6.6	8.7	4.5	3.6	-2.1	5.7	7.0	0.6	6.6

**Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni**

Mwaka	Robo Mwaka	Kilimo	Uchimbaji Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na Maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengen ezo	Malazi na Huduma ya chakula	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2012		16,537,222	3,071,558	5,881,780	522,829	279,326	6,073,134	6,448,378	1,253,970	3,747,784	1,282,255	2,561,997
2013		19,551,225	3,125,480	6,648,876	550,300	324,028	7,921,637	7,063,673	1,317,191	5,246,333	1,433,179	2,541,198
2014		21,313,803	3,097,933	7,533,519	818,693	371,581	8,946,007	8,045,702	1,330,371	6,167,366	1,598,597	3,614,991
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		29,739,111	5,299,362	8,467,126	472,868	433,132	12,264,650	9,861,678	1,523,035	7,549,484	1,739,556	5,268,866
2017		34,154,594	5,206,217	9,102,282	413,351	519,909	14,493,826	10,843,499	1,602,543	7,897,993	1,829,360	4,789,632
2018		36,539,300	6,573,059	10,418,295	348,527	566,562	16,825,564	11,792,072	1,653,792	8,381,276	1,948,116	4,823,650
2012	1	4,401,300	880,216	1,341,018	107,023	64,205	1,443,105	1,595,774	287,270	794,179	277,273	646,245
	2	3,871,082	801,349	1,423,370	132,289	66,277	1,463,179	1,605,723	298,007	929,717	306,370	637,005
	3	2,918,561	839,061	1,536,873	139,411	71,371	1,625,456	1,522,247	336,633	966,819	334,319	650,939
	4	5,346,278	550,932	1,580,519	144,106	77,474	1,541,394	1,724,635	332,061	1,057,070	364,294	627,808
2013	1	5,314,380	772,805	1,481,385	131,753	75,561	1,737,356	1,680,626	325,441	1,052,102	314,712	609,682
	2	4,725,684	757,841	1,574,346	136,360	80,139	1,704,477	1,715,907	316,808	1,359,962	344,060	610,529
	3	3,437,094	762,479	1,843,414	136,734	76,053	2,239,793	1,732,544	341,644	1,415,839	364,619	636,641
	4	6,074,067	832,356	1,749,731	145,453	92,275	2,240,012	1,934,596	333,298	1,418,430	409,787	684,345
2014	1	5,777,094	824,548	1,782,667	199,469	84,281	2,067,401	1,952,932	325,523	1,517,402	345,394	827,517
	2	5,218,700	731,020	1,913,494	182,341	91,657	2,400,626	1,964,773	321,694	1,505,123	389,695	897,349
	3	3,818,738	762,094	2,006,208	214,097	94,135	2,193,995	1,931,017	344,630	1,563,349	429,260	939,942
	4	6,499,270	780,271	1,831,151	222,786	101,508	2,283,985	2,196,980	338,524	1,581,492	434,248	950,183
2015	1	6,327,034	885,335	1,719,164	231,736	98,032	2,304,805	2,059,622	340,826	1,699,272	378,197	961,287
	2	6,213,378	1,014,860	1,932,116	215,874	93,962	2,576,752	2,185,159	346,228	1,695,759	401,697	984,080
	3	4,639,174	989,934	2,055,370	186,369	98,230	2,743,082	2,169,087	375,452	1,702,406	455,031	1,066,915
	4	8,054,973	1,165,491	1,705,021	164,823	100,534	2,822,158	2,333,994	359,411	1,832,458	446,173	1,176,739
2016	1	7,374,976	1,184,525	1,859,359	146,615	97,829	2,907,310	2,380,650	360,730	1,876,790	401,478	1,310,873
	2	7,882,574	1,385,110	2,164,955	119,245	104,927	3,083,464	2,451,490	355,580	1,900,768	402,699	1,329,442
	3	5,411,445	1,388,041	2,185,110	101,557	106,558	3,296,348	2,478,683	398,130	1,891,196	471,727	1,336,256
	4	9,070,116	1,341,686	2,257,702	105,451	123,818	2,977,528	2,550,855	408,595	1,880,730	463,652	1,292,295
2017	1	8,741,604	1,303,539	2,111,981	105,857	111,493	3,321,270	2,560,105	393,360	1,940,809	466,153	1,277,903
	2	9,222,353	1,223,781	2,192,797	95,954	119,956	3,823,828	2,695,873	381,415	1,938,342	458,720	1,223,927
	3	6,018,984	1,290,663	2,476,180	108,353	137,540	3,377,278	2,700,023	413,388	2,012,885	456,117	1,133,422
	4	10,171,654	1,388,234	2,321,323	103,187	150,920	3,971,449	2,887,497	414,380	2,005,958	448,370	1,154,380
2018	1	10,279,854	1,244,714	2,302,826	93,328	118,857	3,941,232	2,740,235	416,104	2,011,217	524,334	1,192,725
	2	10,082,660	1,342,371	2,343,604	90,436	131,424	4,098,635	2,881,172	391,117	2,091,723	508,178	1,194,059
	3	6,271,530	2,498,843	2,809,226	86,042	150,231	3,967,740	2,949,103	432,616	2,108,753	457,905	1,215,224
	4	9,905,256	1,487,131	2,962,638	78,721	166,050	4,817,957	3,221,561	413,955	2,169,583	457,698	1,221,641
2019	1	9,903,760	1,409,686	2,638,234	79,671	135,037	4,608,054	2,847,590	419,290	2,287,724	569,591	1,290,154



**Kiambatisho Na.3 (kinaendelea): Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni**

Mwaka	Robo Mwaka	Utawala na Ulinz	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	Huduma zinazohusiana na Utawala	Upangishaji Majengo	Elimu	Afya na Huduma za Jamii	Huduma nyingine za Kijamii	Jumla ya Ongezeko la Thaman	Ongeza kodi katika bidhaa	Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko
2012		2,882,065	282,744	1,243,365	2,308,221	1,498,868	1,011,197	787,684	57,674,377	4,635,323	62,309,700
2013		3,615,292	353,038	1,522,884	2,551,029	1,728,376	1,113,563	898,918	67,506,219	5,470,981	72,977,200
2014		3,973,787	433,939	1,914,456	2,721,061	2,027,225	1,233,077	1,051,073	76,193,180	6,410,208	82,603,388
2015		4,548,604	518,123	2,183,917	2,949,598	2,413,306	1,419,090	1,144,099	86,484,736	7,864,579	94,349,316
2016		4,846,491	617,914	2,661,978	3,162,290	2,673,289	1,540,484	1,302,342	99,423,658	8,938,667	108,362,324
2017		4,986,287	726,707	3,027,384	3,334,171	2,864,290	1,681,353	1,483,378	108,956,774	9,787,724	118,744,498
2018		5,124,667	817,442	3,306,554	3,553,630	3,081,718	1,812,292	1,628,100	119,194,615	10,169,738	129,364,353
2012	1	654,680	64,487	293,425	554,816	362,966	243,698	184,237	14,195,916	1,072,649	15,268,565
	2	657,485	68,677	303,977	566,007	349,795	254,300	190,456	13,925,065	1,073,834	14,998,898
	3	772,983	72,727	315,854	584,780	392,368	266,923	204,577	13,551,903	1,190,792	14,742,695
	4	796,917	76,853	330,108	602,618	393,739	246,276	208,414	16,001,493	1,298,049	17,299,541
2013	1	828,421	81,453	348,510	623,295	409,442	267,496	213,649	16,268,068	1,272,188	17,540,256
	2	859,486	86,391	370,334	636,658	415,166	282,031	217,725	16,193,902	1,349,405	17,543,307
	3	959,084	90,520	390,731	641,360	448,825	289,666	230,524	16,037,563	1,410,215	17,447,778
	4	968,300	94,674	413,309	649,717	454,943	274,371	237,021	19,006,686	1,439,173	20,445,859
2014	1	941,964	100,534	445,554	660,363	473,455	291,859	251,787	18,869,743	1,525,171	20,394,914
	2	961,320	105,787	470,591	671,001	487,961	309,737	258,097	18,880,966	1,431,265	20,312,230
	3	1,039,034	111,500	492,888	689,078	529,823	316,714	269,694	17,746,196	1,655,211	19,401,407
	4	1,031,469	116,118	505,423	700,619	535,986	314,767	271,495	20,696,275	1,798,561	22,494,836
2015	1	1,044,153	120,964	513,992	726,613	556,940	326,811	274,873	20,569,657	1,656,847	22,226,504
	2	1,067,554	126,516	530,954	730,933	574,920	340,066	278,780	21,309,588	1,937,133	23,246,720
	3	1,221,972	132,595	555,641	738,145	640,268	380,209	292,529	20,442,408	2,054,332	22,496,740
	4	1,214,926	138,048	583,330	753,907	641,178	372,003	297,916	24,163,083	2,216,268	26,379,351
2016	1	1,241,264	143,454	616,445	772,027	674,524	394,067	305,256	24,048,171	2,174,257	26,222,428
	2	1,245,479	150,672	652,116	781,653	679,857	394,612	313,758	25,398,401	2,177,543	27,575,944
	3	1,168,596	158,238	684,007	795,609	652,944	371,218	334,897	23,230,557	2,313,142	25,543,699
	4	1,191,152	165,551	709,411	813,002	665,964	380,587	348,431	26,746,528	2,273,725	29,020,253
2017	1	1,190,207	171,881	729,512	821,402	683,782	398,489	354,711	26,684,058	2,308,930	28,992,988
	2	1,261,790	178,657	749,125	829,673	716,759	428,492	362,229	27,903,672	2,244,906	30,148,578
	3	1,258,467	185,472	768,325	837,161	726,144	419,602	379,621	24,699,625	2,521,183	27,220,809
	4	1,275,824	190,697	780,422	845,934	737,605	434,770	386,817	29,669,419	2,712,704	32,382,124
2018	1	1,291,110	197,629	819,197	858,676	763,386	469,816	390,962	29,656,203	2,476,478	32,132,681
	2	1,248,822	202,968	806,215	880,366	755,523	450,555	401,819	29,901,648	2,403,761	32,305,409
	3	1,288,912	207,101	829,270	900,047	779,402	448,276	413,545	27,813,768	2,661,136	30,474,904
	4	1,295,823	209,743	851,872	914,540	783,407	443,646	421,773	31,822,996	2,628,363	34,451,359
2019	1	1,307,326	217,282	878,759	932,140	803,295	465,936	431,757	31,225,285	2,483,885	33,709,171

**Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa Kwa Bei Za Soko (Bei za miaka inayohusika) -katika asilimia**

Mwaka	Robo Mwaka	Kilimo	Uchimbaji Madini na Maw	Viwanda	Umeme	Maji safi na Maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengenez	Malazi na Huduma ya chakul	Usafirishaji na Uhifadhi mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bim
2012		26.5	4.9	9.4	0.8	0.4	9.7	10.3	2.0	6.0	2.1	4.1
2013		26.8	4.3	9.1	0.8	0.4	10.9	9.7	1.8	7.2	2.0	3.5
2014		25.8	3.8	9.1	1.0	0.4	10.8	9.7	1.6	7.5	1.9	4.4
2015		26.7	4.3	7.9	0.8	0.4	11.1	9.3	1.5	7.3	1.8	4.4
2016		27.4	4.9	7.8	0.4	0.4	11.3	9.1	1.4	7.0	1.6	4.9
2017		28.8	4.4	7.7	0.3	0.4	12.2	9.1	1.3	6.7	1.5	4.0
2018		28.2	5.1	8.1	0.3	0.4	13.0	9.1	1.3	6.5	1.5	3.7
2012	1	28.8	5.8	8.8	0.7	0.4	9.5	10.5	1.9	5.2	1.8	4.2
	2	25.8	5.3	9.5	0.9	0.4	9.8	10.7	2.0	6.2	2.0	4.2
	3	19.8	5.7	10.4	0.9	0.5	11.0	10.3	2.3	6.6	2.3	4.4
	4	30.9	3.2	9.1	0.8	0.4	8.9	10.0	1.9	6.1	2.1	3.6
2013	1	30.3	4.4	8.4	0.8	0.4	9.9	9.6	1.9	6.0	1.8	3.5
	2	26.9	4.3	9.0	0.8	0.5	9.7	9.8	1.8	7.8	2.0	3.5
	3	19.7	4.4	10.6	0.8	0.4	12.8	9.9	2.0	8.1	2.1	3.6
	4											
2014	1	28.3	4.0	8.7	1.0	0.4	10.1	9.6	1.6	7.4	1.7	4.1
	2	25.7	3.6	9.4	0.9	0.5	11.8	9.7	1.6	7.4	1.9	4.4
	3	19.7	3.9	10.3	1.1	0.5	11.3	10.0	1.8	8.1	2.2	4.8
	4	28.9	3.5	8.1	1.0	0.5	10.2	9.8	1.5	7.0	1.9	4.2
2015	1	28.5	4.0	7.7	1.0	0.4	10.4	9.3	1.5	7.6	1.7	4.3
	2	26.7	4.4	8.3	0.9	0.4	11.1	9.4	1.5	7.3	1.7	4.2
	3	20.6	4.4	9.1	0.8	0.4	12.2	9.6	1.7	7.6	2.0	4.7
	4	30.5	4.4	6.5	0.6	0.4	10.7	8.8	1.4	6.9	1.7	4.5
2016	1	28.1	4.5	7.1	0.6	0.4	11.1	9.1	1.4	7.2	1.5	5.0
	2	28.6	5.0	7.9	0.4	0.4	11.2	8.9	1.3	6.9	1.5	4.8
	3	21.2	5.4	8.6	0.4	0.4	12.9	9.7	1.6	7.4	1.8	5.2
	4	31.3	4.6	7.8	0.4	0.4	10.3	8.8	1.4	6.5	1.6	4.5
2017	1	30.2	4.5	7.3	0.4	0.4	11.5	8.8	1.4	6.7	1.6	4.4
	2	30.6	4.1	7.3	0.3	0.4	12.7	8.9	1.3	6.4	1.5	4.1
	3	22.1	4.7	9.1	0.4	0.5	12.4	9.9	1.5	7.4	1.7	4.2
	4	31.4	4.3	7.2	0.3	0.5	12.3	8.9	1.3	6.2	1.4	3.6
2018	1	32.0	3.9	7.2	0.3	0.4	12.3	8.5	1.3	6.3	1.6	3.7
	2	31.2	4.2	7.3	0.3	0.4	12.7	8.9	1.2	6.5	1.6	3.7
	3	20.6	8.2	9.2	0.3	0.5	13.0	9.7	1.4	6.9	1.5	4.0
	4	28.8	4.3	8.6	0.2	0.5	14.0	9.4	1.2	6.3	1.3	3.5
2019	1	29.4	4.2	7.8	0.2	0.4	13.7	8.4	1.2	6.8	1.7	3.8

**Kiambatisho Na. 4 (kinaendelea): Mchango wa Shughuli za Kiuchumi kwa Pato la Taifa Kwa Bei Za Soko (Bei za miaka inayohusika) - katika asilimia**

Mwaka	Robo Mwaka	Utawala na Ulinzi	Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi	Huduma zinazohusiana na Utawala	Upangishaji Majengo	Elimu	Afya na Huduma za Jamii	Huduma nyingine za Kijamii	Jumla ya Ongezeko la Thamani	Ongeza kodi katika bidhaa	Pato la Taifa kwa bei za soko
2012		4.6	0.5	2.0	3.7	2.4	1.6	1.3	92.6	7.4	100.0
2013		5.0	0.5	2.1	3.5	2.4	1.5	1.2	92.5	7.5	100.0
2014		4.8	0.5	2.3	3.3	2.5	1.5	1.3	92.2	7.8	100.0
2015		4.8	0.5	2.3	3.1	2.6	1.5	1.2	91.7	8.3	100.0
2016		4.5	0.6	2.5	2.9	2.5	1.4	1.2	91.8	8.2	100.0
2017		4.2	0.6	2.5	2.8	2.4	1.4	1.2	91.8	8.2	100.0
2018		4.0	0.6	2.6	2.7	2.4	1.4	1.3	92.1	7.9	100.0
2012	1	4.3	0.4	1.9	3.6	2.4	1.6	1.2	93.0	7.0	100.0
	2	4.4	0.5	2.0	3.8	2.3	1.7	1.3	92.8	7.2	100.0
	3	5.2	0.5	2.1	4.0	2.7	1.8	1.4	91.9	8.1	100.0
	4	4.6	0.4	1.9	3.5	2.3	1.4	1.2	92.5	7.5	100.0
2013	1	4.7	0.5	2.0	3.6	2.3	1.5	1.2	92.7	7.3	100.0
	2	4.9	0.5	2.1	3.6	2.4	1.6	1.2	92.3	7.7	100.0
	3	5.5	0.5	2.2	3.7	2.6	1.7	1.3	91.9	8.1	100.0
	4	4.7	0.5	2.0	3.2	2.2	1.3	1.2	93.0	7.0	100.0
2014	1	4.6	0.5	2.2	3.2	2.3	1.4	1.2	92.5	7.5	100.0
	2	4.7	0.5	2.3	3.3	2.4	1.5	1.3	93.0	7.0	100.0
	3	5.4	0.6	2.5	3.6	2.7	1.6	1.4	91.5	8.5	100.0
	4	4.6	0.5	2.2	3.1	2.4	1.4	1.2	92.0	8.0	100.0
2015	1	4.7	0.5	2.3	3.3	2.5	1.5	1.2	92.5	7.5	100.0
	2	4.6	0.5	2.3	3.1	2.5	1.5	1.2	91.7	8.3	100.0
	3	5.4	0.6	2.5	3.3	2.8	1.7	1.3	90.9	9.1	100.0
	4	4.6	0.5	2.2	2.9	2.4	1.4	1.1	91.6	8.4	100.0
2016	1	4.7	0.5	2.4	2.9	2.6	1.5	1.2	91.7	8.3	100.0
	2	4.5	0.5	2.4	2.8	2.5	1.4	1.1	92.1	7.9	100.0
	3	4.6	0.6	2.7	3.1	2.6	1.5	1.3	90.9	9.1	100.0
	4	4.1	0.6	2.4	2.8	2.3	1.3	1.2	92.2	7.8	100.0
2017	1	4.1	0.6	2.5	2.8	2.4	1.4	1.2	92.0	8.0	100.0
	2	4.2	0.6	2.5	2.8	2.4	1.4	1.2	92.6	7.4	100.0
	3	4.6	0.7	2.8	3.1	2.7	1.5	1.4	90.7	9.3	100.0
	4	3.9	0.6	2.4	2.6	2.3	1.3	1.2	91.6	8.4	100.0
2018	1	4.0	0.6	2.5	2.7	2.4	1.5	1.2	92.3	7.7	100.0
	2	3.9	0.6	2.5	2.7	2.3	1.4	1.2	92.6	7.4	100.0
	3	4.2	0.7	2.7	3.0	2.6	1.5	1.4	91.3	8.7	100.0
	4	3.8	0.6	2.5	2.7	2.3	1.3	1.2	92.4	7.6	100.0
2019	1	3.9	0.6	2.6	2.8	2.4	1.4	1.3	92.6	7.4	100.0